

Maswali

1. Yeroboamu alikuwa mfalme mzuri au mbaya?
2. Mbona Waisraeli walichagua Yeroboamu kama mfalme wao?
3. Yeroboamu aliweka wapi wale ndama wawili wa dhahabu?
4. Nini ilifanyika Yeroboamu alipojaribu kumnyamazisha mtu wa Mungu?
5. Mkono wake uloponaje?
6. Mbona mtu wa Mungu hakukula au kukunywa na Yeroboamu?
7. Mtu wa Mungu alikufaje?
8. Nani alienda kwa Ahiya akasaidie Abiya?
9. Mbona Ahiya hakumsaidia Abiya?
10. Mbona Waisraeli wote walihuzunika Abiya alipokufa?

Majibu

1. Mfalme mbaya.
2. Kwa sababu hawakupenda vile Rehoboamu aliwatawala.
3. Aliweka moja Betheli na mwingine Dani.
4. Mkono wake ulinyauka na kupooza na madhababu yalivunjika kwa vipande.
5. Aliambia mtu wa Mungu akamuomba kwa Mungu akapona.
6. Kwa sababu Mungu alikuwa amemuonya asikule.
7. Simba alimuua.
8. Mke wa Yeroboamu alienda kwa udanganyifu.
9. Kwa sababu ya uovu uliofanywa na Yeroboamu.
10. Kwa sababu Abiya alikuwa mtu mzuri.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



21 Yeroboamu

Marejeo

1 Wafalme 12—1 Wafalme 14:20

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu ana uwezo hata tukifikiria tunaweza



Maneno maalum

1. Yeroboamu + mfalme + Israeli + dhambi.
2. Rehoboamu + Yuda + Israeli + ndama wawili wa dhahabu + Betheli + Dani + abudu sanamu.
3. Dhabihu + mtu wa utauwa + mkono + madhabahu.
4. Chakula + nabii mzee + danganya + simba.
5. Abiya mgonjwa + nabii Ahiya + geuza (badilisha).

21.1 Yeroboamu alikuwa mfalme wa kwanza wa Israeli. Alitawala kwa miaka 22 lakini alikuwa mfalme mbaya. Mara nyingi kwa kitabu cha wafalme, tunasoma hiki kifungu, “Yeroboamu mwana wa Nebati aliyefanya Waisraeli wakatenda dhambi.”

21.2 Yeroboamu alikuwa mfalme kwa sababu watu hawakufurahia utawala wa mfalme Rehoboamu. Wakamfanya Yeroboamu awe mfalme juu ya Israeli. Kulikuwa na mgawanyiko – Rehoboamu alitawala nchi ya Yuda na Yeroboamu nchi ya Israeli. Kwa sababu watu wake wengine walienda kuabudu Mungu Yerusalemu, Yeroboamu alikuwa na hofu. Alifikiria kwamba mwishowe hao watu watarudi kwa mfalme Rehoboamu. Alitengeneza ndama wawili wa dhahabu na akawaambia Waisraeli, “Yerusalemu ni mbali sana kuenda

kutoa dhabihu. Kuna hapa miungu miwili walioletwa kutoka Misri, kwa hivyo abuduni hawa.” Aliweka mmoja kwa nchi ya Kaskazini kwa mji wa Dani na mwingine Betheli Kusini mwa nchi. Hili lilikuwa jambo mbaya sana. Watu walianza kuziabudu sanamu badala ya kumwabudu



Mungu. Pia Yeroboamu aliwaandalia watu wa Israeli karamu za kidini. Aliziandaa hizi karamu kwa siku tofauti na za dini ya Yuda.

21.3 Siku moja wakati Yeroboamu alikuwa anafanya dhabihu kwa sanamu yake, mtu wa Mungu kutoka Yuda alimtokea. Alimwambia kwamba Mungu anaenda kufanya ishara

Mfalme Yeroboamu hakufurahia, akainua mkono na kupasa sauti akisema, “Mkamate!” Alipofanya hivyo, mkona wake ukanyauka ukapooza tena madhabahu yakavunjika kwa vipande, kama ishara vile mtu wa Mungu alisema. Mfalme Yeroboamu akaambia huyo mtu amuombee kwa Mungu ili apone mkono wake. Alimwombee na mkono ukapona.

21.4 Yeroboamu alifurahi na kuuliza mtu wa Mungu akule chakula naye. Huyo mtu akajibu, “Hata ukinipa nusu ya ufalme wako, sitakula au kunywa. Mungu amenikanya na kuniambia hata kuenda nitaendea njia nyingine.” Na akaondoka arudi nyumbani. Nabii mzee aliposikia maneno ya mtu wa Mungu alienda kukutana naye akamdanganya akisema, Mungu alikuwa amemwambia warudi kwa nyumba yake wakale. Mtu wa Mungu alifanya hivyo, walipokuwa wakila, Mungu alizungumza na nabii mzee, alimwambia amwambie mtu wa Mungu kwamba amemuasi kwa kukula kwa hivyo ataadhibiwa. Baada ya kula aliondoka kuenda nyumbani. Lakini njiani alikutana na simba na akamuua.



21.5 Kwa wakati huo huo, Abiya mwana wa Yeroboamu akaanza kuwa mgonjwa. Yeroboamu aliambia mke wake aende atafute usaidizi kutoka kwa nabii Ahiya. Alitakiwa ajigeuze asijulikane, lakini alipofika kwa nyumba ya Ahiya, alimtambua kwa sababu Mungu alikuwa amemwambia. Alimwambia kwamba Abiya hatapona kwa ajili mfalme Yeroboamu alimfanyia Mungu maovu. Alimwambia mwanao atakufa tu utakapofika nyumbani na hivyo ndivyo ilivyokuwa. Aliporudi tu, mwanawe Abiya akafa. Waisraeli wote walihuzunika kwa sababu alikuwa mtu mzuri. Baada ya mda mfupi, mfalme Yeroboamu naye alikufa na mwanawe Nalabu akawa mfalme.